

Chekechea bila mianasesere

Taarifa kwa wazazi

Kwa miezi 3, mianasesere itakuwa likizoni - viti vyao vitabaki, meza, kamba, vibanio, boksi la karatasi nene... ubunifu wa watoto na watoto wenyewe.

Lengo la mradi huu ni nini?

Watoto wanapata muda zaidi wa kucheza kwa uhuru zaidi kwenye chekechea isiyo na mianasesere. Wanatumia akili zao kuamua ni kitu gani wanachotaka kufanya. Mawazo ya kufanya shughuli yanatokana na watoto hao. Stadi muhimu za maisha zinaboreshwa: mazungumzo baina yao, kutatua matatizo kwa pamoja, waking'amua nini wanachokitaka wao, wakihihi namna wengine wanavyojisikia, wakijifunza kujadiliana vyema.... ujuzi ambao unahitajika ili kukua kufikia kuwa vijana wenye kujitegemea na watu wazima.

Watoto watajifunza nini kutoka kwenye mradi?



Kuunda vitu

Ninawezaje kupanga viti bila ya kuangusha kila kitu? Hii inamaanisha kujifunza namna kanuni za mazoezi ya viungo zinavyofanya kazi kupitia kucheza.

Watoto aghalabu hupanga miradi ya ujenzi baina yao. Wanajizoesha kuchangia mawazo kwenye kundi, kuwa msimamizi/kiongozi na kufikia maridhiano. Kucheza pamoja badala ya upande kwa upande! Hiyo inahitaji mazoezi.

Kula asusa muda wa katikati ya asubuhi

Ninasikia kiu, njaa, kuchoka au ninahitaji kula kwa sasa kwa vile hiki ndicho marafiki wawili wanachokifanya? Kwenye chekechea bila mianasesere watoto wanaweza kuamua wenyewe wakati gani na wapi wanataka kula asusa zao za muda wa katikati ya asubuhi. Hii inaruhusu watoto kujifunza kufahamu hisia za miili yao, na kutafakari utashi wao kijamii kama vile "kula pamoja".

Kujadiliana na kuelewana

Watoto hao wanajifunza kueleza maoni yao wenyewe na kujitetea kwa dhati. Kujiamini zaidi na kwa uwazi kabisa kuweza kuunda matakwa yao kwa uwazi. Wanajifunza kuelezea hisia zao, wakikuza msamiati wao kwa utaratibu.

Kujisikia kuchoshwa

Yawezekana kabisa kuwa watoto wanaweza kujisikia kuchoshwa na mazungumzo wakati fulani. Kwenye chekechea isiyo na mianasesere, mwalimu wa chekechea anajizuia na kumpa mtoto

muda wa kutafuta njia ya kuepukana na kuchoshwa huko. Wakati mwingine ni SAWA kukaa tu na kuangalia kinachoendelea na kukodolea macho angani. Watoto wanahimizwa kutunga wazo la mchezo mpya kwa ajili yao. Uchoshi aghalabu ndio unaozaa ubunifu.

Kuwa jasiri zaidi

Kupitia michezo, watoto hujipa fursa ya kuepukana na woga na kuwa jasiri zaidi. Hii yaweza kumaanisha kuruka kutoka mezani hadi chini kwenye mkeka. Watasita iwapo mkeka upo mbali sana au kama watoto wengine bado wapo kwenye huo mkeka. Wataomba msaada, kushuka chini tena na kuusogeza mkeka karibu zaidi au kujenga “jukwaa la kuchupia” lililo juu zaidi. Wanapanda, kuruka, kutambaa, kudansi... Wanajifunza kupima uwezo wao na kutathmini vikwazo vyema zaidi ili kupunguza kujiimiza wao wenyewe au wengine.

Asubuhi ya kawaida ya chekechea inakuwaje?

Watoto hufika chekechea, kubadilisha nguo wao wenyewe kwenye chumba cha kuhifadhia nguo/makoti, kumwamkua mwalimu wao, kisha huenda kucheza. Wengine huja chekechea wakiwa na wazo thabiti la nini wanachotaka kufanya, au kuendelea kucheza walipoishia jana. Wengine hutembea kuzunguka chekechea hiyo ili kupata wazo au mchezo. Wengine hukaa chini na kutazama kinachoendelea. Watakula watakaposikia njaa au kuhisi kama wanataka kula. Karibu na mwisho wa nusu-siku, majadiliano yanafanyika na uamuzi kufikiwa wa jinsi gani na nini cha kuweka sawa. Baadaye mwalimu wa chekechea hufanya tathmini ya asubuhi hiyo na watoto. Kitu gani mlifikurahia zaidi leo? Kitu gani hasa kinakufanya ujisikie na fahari?

Chekechea isiyo na mianasesere: je, hii inamaanisha hakuna sheria?

La hashu. Sheria za kawaida za chekechea kwa ujumla zitaendelea kutumika. Zingine zitabadilika kidogo. Watoto wanapewa nafasi ya kuamua zaidi. Baadhi ya taratibu pia hufuatwa, wakati ambapo nyingine hubadilika.

Jukumu la mwalimu ni nini?

Mwalimu wa chekechea anaambatana na watoto hao kwa kujizuia, akiwawezesha kiasi kikubwa kukuza ujuzi wao. Wanaendelea kuona kinachoendelea kwenye chekechea hiyo na kupata utambuzi wa ndani zaidi wa kiwango cha ukuaji wa watoto hao. Huwaongoza watoto ili waanze kufikiri kwa ajili yao wenyewe. Watoto hujifunza mengi kwa kusikilizwa wanachokitaka, kwa kuhusishwa jinsi ya kupanga vitu, kwa kuchangia mawazo na kwa kuwajibika.

Vipi ikiwa ninahofia kuhusu mtoto wangu?

Iwapo unahofia kuhusu kitu fulani au kama mtoto wako hataki kwenda chekechea, tafadhali wasiliana na mwalimu wa chekechea ili majadiliane uliyoyaona na mashaka yako.

Chekechea ya Aargau yenye kujikinga dhidi ya uraibu na isiyo na mianasesere?

Kujikinga dhidi ya uraibu kwa Aargau ilizindua mradi kwenye mkoa wa Aargau mnamo 2002 na imekuwa ikiendeshwa nao tangu wakati huo. Watu wenye ujuzi mzuri wa maisha ni vigumu kuanza tabia za kiraibu. Hutafuta suluhisho pale wanapokutana na hali tete kimaisha na ni wazuri wa kutafuta na kupokea msaada. Wanajitambua na wanajua nini wanaweza kufanya. Wanaweza kupata maneno ya kuelezea namna wanavyojisikia.

Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika www.spielzeugfrei.ch